

**R**AIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Dk. Stergomena Tax, kuwa Mbunge wa

Bunge

wa Tanzania.  
Spika Job Ndugai, alimwapisha jana kabla ya shughuli zingine za Bunge kuendelea.

Taarifa iliyotolewa jana kwa

na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Jaffar Haniu, Dk. Stergomena ameteuliwa kutoka katika nafasi 10 za wabunge wa kuteuliwa na Rais.

Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambaye amemaliza muda wake Agosti, mwaka huu.

# \*RC Dar aduwazwa kusuasua machinjio ya Vingunguti

UHURU UK 4

## Na CHRISTOPHER LISSA

MKUU Wa Mkoa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameonyeshwa kuduwazwa na kusuasua kwa mchakato wa umalizaji wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti.

Makalla aliyasema hayo jana alipotembelea machinjio hayo.

Hiyo ni mara ya pili kwa mkuu wa mkoa huyo kufanya ziara katika eneo hilo.

"Mradi huu ulikuwa katika bajeti ya awamu ya tano na kuendelea awamu ya sita kwa matarajio ya kuchinja ng'ombe

1000, mbuzi 1000 na kondoo 500 kwa siku, kwa ajili ya soko la ndani na kusafirisha nchi zingine hasa Oman na Dubai.

"Mchanjio hayo hayajaanza kufanya kazi kwa sababu ya kukosa chumba cha baridi (cold room) cha kuhifadhi nyama hizo, hivyo haiwezi kutumika," alisema.

Alimshauri Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuusimamia mradi huo hadi utakapoanza kufanya kazi.

Alisema alitarajia machinjio hayo angeyakuta yameanza kufanya kazi ya kuchinja ng'ombe, kondoo na mbuzi kwamba, kilichokamilishwa ni majengo.

"Nilikuwa nafuatilia ahadi kwa Waziri Mkuu iliyotolewa na watendaji wa machinjio, alitarajia kufika Julai Mosi, ungekuwa umekamilika na mimi nilipokuja, mliniahidi Julai 27, mwaka huu utakuwa umekamilika kwa sasa naona hali ni ile ile," alisema.

Makalla alimwambia Kaimu Mkurungezi wa Jiji la Ilala, Tabu Shaibu na timu ya manunuzi kukaa kikao na kutafuta mkandarasi atakayekamilisha ununuza wa vifaa vinavyohitajika ili chumba cha baridi kikamilishike, kianze kufanya kazi kama yalivyo matarajio ya wananchi.

Kwa upande wake, Kaimu

Mkurugenzi wa Jiji alitoa ahadi kwa mkuu wa mkoa kwamba, ifikapo Septemba 13, mwaka huu, watakuwa wamepata mkandarasi ili aendelea na mikakati mingine ya ununuza wa vifaa hivyo nje ya nchi na kukamilisha chumba cha baridi.

## MCHAKATO

## MACHINJIO

Alitarajia machinjio hayo angeyakuta yameanza kufanya kazi ya kuchinja ng'ombe...